



TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA KUWANIA TUZO ZA SHIRIKA LA MILIKI UBUNIFU DUNIANI KWA MWAKA 2024 (2024 WIPO GLOBAL AWARDS)

Dar es Salaam - 1 Februari, 2024

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imepokea mwaliko kutoka Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) kwaajili ya wafanyabiashara wa Tanzania kuwania Tuzo za WIPO kwa Mwaka 2024. Muda wa kutuma maombi ni kuanzia Januari 15 hadi Machi 31, 2024.

Tuzo za WIPO zinatolewa kimataifa, na zinalenga kusherehekea na kutambua mchango wa wajasiriamali wadogo na wakati, (SMEs) katika kutumia Miliki Ubunifu katika uendeshaji wa biashara, na kuleta mabadiliko chanya kiuchumi, na kijamii kwa ujumla.

BRELA inawahamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati kuchangamkia fursa hii na kushiriki katika kinyang'anyiro cha *2024 WIPO Global Awards* katika sekta zote za uchumi kama; nyanja ya kiteknolojia, kilimo, viwanda vya ubunifu au nyanja nyingine na kutuma maombi ili kupata tuzo hizo.

Maombi yanaweza kutumwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kirusi au Kijapani. Jopo la Waamuzi litachagua hadi washindi saba watakaoalikwa kuhudhuria hafla ya Tuzo wakati wa Mkutano Mkuu wa WIPO utakaofanyika Julai, 2024 Geneva Uswisi.

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Tuzo za WIPO Duniani <https://www.wipo.int/global-awards/en/how-to-apply.html> na kwa usaidizi zaidi wasiliana nasi kupitia simu namba +255 (0) 22 221 2800

**IMEANDALIWA NA:
KITENGO CHA UHUSIANO**